BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Kwanza – Tarehe 25 Novemba, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 19 Septemba, 2026.

1. Toleo Namba 7391 la tarehe 22 Agosti, 2025;
2. Toleo Namba 7420 la tarehe 14 Novemba, 2025;
3. Toleo Namba 7448 la tarehe 13 Machi, 2026;
4. Toleo Namba 7484 la tarehe 20 Mei, 2026;
5. Toleo Namba 7526 la tarehe 18 Agosti, 2026;
6. Toleo Namba 7530 la tarehe 18 Agosti, 2026;
7. Toleo Namba 7531 la tarehe 18 Agosti, 2026;
8. Toleo Namba 7523 la tarehe 4 Septemba, 2026;
9. Toleo Namba 7524 la tarehe 11 Septemba, 2026;
10. Toleo Namba 7527 la tarehe 11 Septemba, 2026;
11. Toleo Namba 7528 la tarehe 11 Septemba, 2026;
12. Toleo Namba 7529 la tarehe 11 Septemba, 2026;
13. Toleo Namba 7533 la tarehe 18 Septemba, 2026;
14. Toleo Namba 7534 la tarehe 18 Septemba, 2026;
15. Toleo Namba 7535 la tarehe 18 Septemba, 2026;
16. Toleo Namba 7536 la tarehe 18 Septemba, 2026;
17. Toleo Namba 7538 la tarehe 2 Oktoba, 2026; na
18. Toleo Namba 7539 la tarehe 2 Oktoba, 2026;

Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Nam. 8 ya 2005 na Kutunga Sheria ya Usalama na Afya Kazini kwa ajili ya kuhakikisha usalama, afya na ustawi wa watu kazini na kuwalinda watu wengine dhidi ya hatari zinazotokana na shughuli za kazi na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Uwekezaji:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi na Uwekezaji Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Nam. 8 ya 2005 na Kutunga Sheria ya Usalama na Afya Kazini kwa ajili ya kuhakikisha usalama, afya na ustawi wa watu kazini na kuwalinda watu wengine dhidi ya hatari zinazotokana na shughuli za kazi na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo

III. MASWALI:

1. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Swali Nam.132: **MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete)** - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Tarehe 9 Aprili 2026, ulivuma upepo mkali sana ulioleta madhara makubwa kwa baadhi ya sehemu ndani ya jimbo la Wete, kwa takribani nyumba zisizopunguwa ishirini na tano zilikumbwa na maafa hayo, ingawaje hadi leo hii Serikali bado haijakuchukua hatua yoyote.

Ni lini Serikali itawasaidia wananchi waliokumbwa na janga la kupoteza nyumba zao kwa kuezuka na upepo.

2. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Swali Nam. 91: **MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole)** - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Wakala wa Ulinzi wa JKU ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria na imeajiri vijana wazalendo ambao wanajitolea katika

kulijenga Taifa.

Ni sababu zipi zinazopelekea vijana hao wanaojitolea na kukubali kulipwa mshahara mdogo kwa maslahi ya Taifa, kuchelewa na kutolipwa kiwango kidogo cha kujitolea kwao na baadhi yao kufikia hadi miezi ishirini na mbili bila ya malipo.

3. <u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>

Swali Nam.11: MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Eneo la Mjini Wingwi linatumika sana kuchimba mawe na fusi na kuna wakati wachimbaji hutumia tambi za mabomu ama baruti.

(a) Je, Serikali imefanya tathmini yoyote ya athari za uchimbaji huo.

(b) Je, Serikali imewahi kukaa na wananchi wa Wingwi kujadiliana juu ya taharuki kubwa inayopatikana kwao, kutokana na uchimbaji wa kutumia mabomu na baruti.

(c) Je, ni lini Serikali itatumia njia nyengine mbadala ya uchimbaji wa rasilimali hizi ukiacha hiyo inayotumika sasa.

4. <u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

Swali Nam.103: MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wazazi na walezi wamekuwa wakibeba gharama mbalimbali za kambi za wanafunzi, hali inayoongeza mzigo wa gharama za elimu kwa familia.

(a) Kwa kiasi gani Serikali inatambua uwepo wa ada au michango wanayotozwa wanafunzi kwa ajili ya kambi katika skuli mbalimbali.

(b) Ni utaratibu gani unaotumika kuidhinisha kiwango cha ada au michango hiyo.

(c) Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha ada za kambi

haziwi mzigo kwa wazazi wala sababu ya mwanafunzi kushindwa kushiriki katika shughuli muhimu za kielimu.

5. <u>Wizara ya Afya:</u>

Swali Nam.14: **MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) -** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kampuni ya NSK imepewa kazi ya uendeshaji wa Hospitali ya Lumumba na wanalipwa kila mwezi kutokana na huduma hizo.

(a) Je, NSK wanao uzoefu wa kuendesha hospitali kubwa na kama wanao ni hospitali gani kubwa waliyowahi kuiendesha Tanzania.

(b) Je, ni malipo ya kiasi gani kwa mwezi kampuni hiyo inalipwa katika uendeshaji wa hospitali ya Lumumba.

(c) Mpango gani umewekwa wa kuhamisha utaalamu kutoka kwa NSK kwenda kwa wataalamu wazawa na je mpango huo unatekelezwa vipi.

Swali Nam.64: **MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) -** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ina mpango gani wa kudhibiti uuzaji wa dawa za sumu ya panya zinazouzwa kiholela bila ya utaratibu maalum.

Swali Nam.122: **MHESHIMIWA MOZA MOHAMMED KHAMIS (Nafasi za Wanawake)** - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika hospitali ya Abdala Mzee Pemba, kumezuka tabia mbaya ya ukiukwaji wa maadili ya kazi kwa baadhi ya madaktari kuwafanyia vitendo visivyo vya kimaadili wagonjwa wa kike na kupelekea wagonjwa hao kutokuwa na imani na madaktari hao kwa kuogopa kabisa kutibiwa katika hospitali hiyo.

(a) Je, ni hatua gani Serikali itachukua kuhakikisha madaktari hao wanajuilikana, wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuchukuliwa hatua za kisheria.

(b) Kwa kiasi kipi Serikali ipo tayari kushirikiana na wananchi waliofanyiwa vitendo hivyo, ili kuhakikisha

nidhamu na uadilifu katika tiba unapatikana.

6. Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Swali Nam. 29: MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Uimarishaji wa huduma za mifugo, hususani kupitia ujenzi wa vituo vya kisasa vya matibabu na ushauri wa kitaalamu, ni muhimu katika kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya mifugo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya kisasa vya matibabu ya mifugo, ili kuboresha huduma kwa wafugaji.

(b) Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa kuhakikisha upatikanaji wa wataalamu wa mifugo na huduma za ushauri wa kitaalamu katika vituo hivyo.

Swali Nam. 65: MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Punda ni mnyama ambae, pamoja na matumizi mengine, hutumika kwa ubebaji wa mizigo na hata kuwa sehemu ya maonesho kwa watalii wetu.

Ni upi uhifadhi na matumizi sahihi wa Wanyama Punda katika miji yetu.

7. Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Swali Nam. 111: MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Pamoja na Serikali kukusudia kupanua na kuongeza nguvu kwenye michezo kwa kujenga viwanja vya mpira vya kisasa, hadi sasa ndani ya Kisiwa cha Pemba ni Uwanja wa Gombani pekee ndio uliojengwa.

(a) Ni lini Serikali itavijenga viwanja vya mpira vya Pemba kama ilivyovijenga vya Unguja.

(b) Ni lini viwanja vya mpira katika Jimbo la Wete vitajengwa, huku ikifahamika kuwa ndio sehemu ambayo mpira wa miguu unapendwa zaidi.

8. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:

Swali Nam. 7: MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Licha ya Serikali kuhakikisha kuwa kunakuwa na mashirikiano baina ya Mawizara na ushirikishwaji wa Wadau mbalimbali katika ujenzi wa barabara kwa lengo la kulinda miundombinu iliyokuwepo. Hata hivyo, Mkandarasi aliyejenga barabara ya *Felix Moumie* ndani ya Jimbo la Malindi amefukia chemba (*man-hole*) za maji taka pamoja na mitaro ya maji taka iliyopo kwenye barabara hiyo, jambo ambalo limesababisha maji taka kuzagaa mitaani, hususan mitaa ya Gulioni.

(a) Je, kwa nini Mkandarasi huyo ameiziba mitaro hiyo, licha ya kushiriki kwa Wadau mbalimbali wakati wa ujenzi, pamoja na kuwepo utaratibu na utambuzi wa mitaro hiyo.

(b) Je, Wizara imechukua jitihada gani katika kumsimamia Mkandarasi kufukua na kujenga chemba hizo, ambapo jitihada ya kurudisha ikionekana kusuasua.

Swali Nam. 47: MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Sheria zinazohusiana na Usalama wa Barabarani zinamkataza dereva wa chombo husika kuendesha chombo hicho kwa mwendo wa kasi au akiwa amelewa.

Je, ni hatua gani zinazochukuliwa dhidi ya madereva wanaoendesha vyombo vya moto barabarani kwa mwendo wa kasi au wakiwa wamelewa.

Swali Nam. 109: MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa Zanzibar ni kitovu cha masuala ya ubaharia na vijana wake wengi wameshawishika na kujikita katika

harakati hizo. Vijana hao hadi leo hii wanahangaika kwenda kutafuta Chuo Tanzania Bara, wakati walitamani huduma hiyo ipatikane Zanzibar.

Ni lini Serikali itajenga Chuo kikubwa Zanzibar tena cha Kimataifa cha kusomeshea Mabaharia Wazawa na hata wa Kigeni.

9. <u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>

Swali Nam. 157: **MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) -** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Asilimia 80 (80%) ya wakaazi wa jimbo la Tumbe ni wavuvi, ingawaje hadi leo hii wanaendelea na shughuli zao za uvuvi bila ya kuwa na chombo cha uokozi.

Kwa kiasi gani Serikali inalishughulikia tatizo hili.

IV. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji:</u>

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Nam. 8 ya 2005 na Kutunga Sheria ya Usalama na Afya Kazini kwa ajili ya kuhakikisha usalama, afya na ustawi wa watu kazini na kuwalinda watu wengine dhidi ya hatari zinazotokana na shughuli za kazi na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
25 Novemba, 2026.

(Hassan A. Haji)
KATIBU,
BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR.